Tangazo hili limeidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji Na Dhamana (CMSA)

**iTRUST FINANCE LIMITED**

(Imepewa Leseni na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) ya kutoa huduma ya Utendaji katika masoko ya mitaji, Usimamizi na Ushauri wa Uwekezaji: iTrust EAC Large Cap ETF imesajiliwa na CMSA kama Mfuko wa Uwekezaji (ETF), Namba ya usajili namba I0074/F07)

# TAARIFA KWA UMMA

iTrust Finance Limited inatoa taarifa kwa umma kuwa mnamo tarehe 28 Oktoba 2025 Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania, imeidhinisha Waraka wa Toleo (Offer Document) na Mkataba wa Uendeshaji wa Mfuko wa iTrust EAC Large Cap ETF (Mfuko utakaowekeza kwenye hisa za kampuni zilizoorodheshwa kwenye masoko ya hisa ya nchi za Afrika Mashariki). CMSA imeidhinisha Mfuko wa iTrust EAC Large Cap ETF kuendeshwa na iTrust Finance Limited kama Meneja wa Mfuko na Benki ya NBC kama Mtunza Dhamana wa Mfuko. iTrust Finance Limited ina leseni kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kwa ajili ya Usimamizi wa Uwekezaji, Uwakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam, na Ushauri wa Uwekezaji.

## MUHTASARI WA TAARIFA MUHIMU ZA MFUKO WA iTRUST EAC LARGE CAP ETF

Sifa Muhimu za iTrust EAC Large Cap ETF

| | | |
|---|---|---|
| (a) | Kiasi cha Toleo | TSH 10,000,000,000 |
| (b) | Sera ya Uwekezaji | Mfuko utawekeza kwenye hisa za kampuni zilizoorodheshwa katika masoko ya hisa ya nchi za Afrika Mashariki, ambazo zina mitaji mikubwa (Large Market Cap) na utendaji mzuri zaidi. |
| (c) | Bei ya Mauzo | Vipande vitauzwa kwa bei ya TSH 1,000 kwa kila Kipande wakati wa Mauzo ya Awali |
| (d) | Kiwango cha Chini cha Uwekezaji wa Awali | Kiwango cha chini ni vipande 100, sawa na TSH 100,000 |
| (e) | Matumizi ya Fedha | Kuwekeza katika hisa za kampuni zilizoorodheshwa kwenye masoko ya hisa ya nchi za Afrika Mashariki, ambazo zina mitaji mikubwa na utendaji mzuri zaidi. |
| (f) | Ukwasi | iTrust EAC Large Cap ETF itaorodheshwa kwenye wenye Soko la hisa la Dar es Salaam (DSE) na wawekezaji wataruhusiwa kununua na kuuza Vipande kwa bei ya soko wakati wote wa siku ya biashara. |

**RATIBA YA MAUZO YA AWALI**

| Tukio | Tarehe |
|---|---|
| Ufunguzi wa Mauzo | 17 Novemba, 2025 |
| Kufungwa kwa Mauzo ya Awali | 12 Desemba, 2025 |
| Kukamilika kwa Orodha ya Usajili | 19 Desemba, 2025 |
| Kutangazwa kwa Matokeo | 05 Januari, 2026 |
| Taarifa ya Matokeo | 05 Januari, 2026 |
| Kuwasilishwa kwa Orodha ya Usajili CSDR | 05 Januari, 2026 |
| Usajili wa Akaunti za CDS | 09 Januari, 2026 |
| Uorodheshaji wa ETF kwenye soko la hisa | 13 Januari, 2026 |
| Ufunguzi wa Ununuzi na Uuzaji wa vipande kwenye soko la hisa | 13 Januari, 2026 |

Wawekezaji wanaweza kuwekeza kwa njia ya kielektroniki kwa kujaza fomu ya maombi inayopatikana kwenye tovuti www.itrust.co.tz, kwenye ofisi ya iTrust Finance Limited, matawi ya Benki ya NBC na ofisi za Mawakala wa Soko la Hisa la Dar es salaam wenye leseni kutoka CMSA.

Wawekezaji wanashauriwa kuwasiliana na mawakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam wenye leseni kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA); wahasibu, wanasheria au washauri wengine wa masuala ya fedha kwa ushauri elekezi ili kufanya maamuzi sahihi ya uwekezaji.

**Imetolewa na:**
**Afisa Mtendaji Mkuu,**
**iTrust Finance Limited,**
**S. L. P. 22636, 429 Mahando Street,**
**Masaki, Dar es Salaam, Tanzania**
**Simu: +255 659 071 777, Barua pepe: info@itrust.co.tz, Tovuti: www.itrust.co.tz**

**Tarehe: 17 Novemba 2025**

Tangazo hili limetolewa kwa idhini ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kwa mujibu wa kanuni za Masoko ya Mitaji za Matangazo, G.N. Namba. 15 ya mwaka 1997.